**Learning by Ear 2011 – Road Safety**

**Episode 05 – Vehicle Maintenance**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Martin Vogl**

**CHARACTERS:**

Onyesho la 1:

- EVANS (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 40-50)
- SAMUEL (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)

Onyesho la 2:

- SAMUEL (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)
- DRIVER (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 25-35)
- MTEMBEA KWA MIGUU (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 50-60)
- JOHN (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)
- ASKARI POLISI (MWANAMUME)

Scene 3:

- FUNDI MAGARI (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 40-50)
- SAMUEL (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)

Intro/Studio/Outro:

- MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)
- GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME)

**Intro:**

**1. Beatrice:** Hujambo, jina langu ni Beatrice na karibuni kwenye makala yetu ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani. Kwenye vipindi vyetu vyote kumi tunaandamana na familia ya Wanjiru. Tunaangazia maisha yao ambapo walishuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Tunazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tujue jinsi ya kuhakikisha usalama zaidi barabarani kwa lengo la kuokoa maisha. Katika kipindi kilichopita jamaa waljumuika kula chajio kwa mara ya kwanza tangu ajali zilipotokea. Mazungumzo yaliyoanza kuhusu usalama barabarani yanaishia kuwa mzozo wa kifamilia wakati ambapo Alice na Nelson wanapogundua kwamba baba yao hana kibali halali cha kuendesha magari.

Katika kipindi hiki, Samuel anaamua kufanya mtihani wa kuendesha gari ili apate kibali halali. Anaelekea kwenye kituo cha kuendesha magari lakini nusura akose kufika huko kwa kuwa basi lake halimo katika hali nzuri.

**Scene One: Neighbour's house**

**2. SFX Atmo:** **Cooking**

**3. EVANS:** Na nikikukopesha fedha itakubidi unilipe kiasi fulani kila mwezi kwa muda wa miezi mitano – natumai hivyo ni sawa, Samuel? Aah na pia ni lazima unionyeshe kibali chako mara utakapokipata.

**4. SAMUEL:** Bila shaka, Evans – Ni kwa sababu ya ya familia yangu ndipo ninataka kupata kibali halali. Nitakurejeshea fedha zako, usiwe na shaka.

**5. EVANS:** Hizi hapa!

**6. SFX:** **hands over notes of money)**

**7. SAMUEL:** Asante sana. Nakwenda sasa hivi kujisajili kwa mafunzo ya kuendesha gari. Tutaonana baadaye, Evans. Ninakushukuru kwa yote!

**8. SFX:** **Opening door and leaving. Sound of car starting up outside**

**<u>Scene Two: Driving in the mini bus</u>**

**9. SFX Atmo:** **Mini bus running on the roads**

**10. SAMUEL:** Hilo ni tatizo moja ambalo limepata ufumbuzi … Imebaki sasa mimi kwendelea na mafunzo ya udereva na kupata kibali cha kuendesha magari. Nadhani askari polisi watazingatia juhudi zangu za kujaribu kuwa dereva bora… Aaah balaa nyingine tena ya msongamano wa magari… Kuna nini… breki za gari zina nini? Mbona halisimami… Simama, simama!!!

**11. SFX:** **crunch of mini bus hitting back of stationary car**

**12. SFX:** **car doors opening**

**13. DRIVER:** **(shouting)** Unafanya nini? Unajua vyema unatakiwa kusimamisha gari nyuma yangu na si kuligonga!

**14. SAMUEL:** Samahani, pole… Gari lako limeharibika? Nimejaribu kusimamisha langu lakini breki zake zimekwama… Gari lako limeharibika?

**15. DRIVER:** Ninaangalia… Una bahati umegonga chuma …Lakini basi lako limebonyeka… **(with irony)** Una bahati sana! Acha nende zangu kazini. Fanya bidii utengenezewe hizo breki jamaa!

**16. SFX:** **Car doors opening and closing. Car starting and driving off**

**17. SAMUEL:** Shida nyingine hiyo. Sijui hizi breki zina nini… afadhali nilipeleke hili gari kwenye karakana punde nitakapomaliza kujisajili kwa mafunzo ya udereva.

**18. SFX:** **Starting up mini bus… Driving along… Sound of mini bus lurching a bit... Tyre popping**

**19. SAMUEL:** Mbona tena?! Kwani hili gari lina nini?

**20. SFX:** **Turns off engine, opens door and gets out)**

**21. SAMUEL:** Mungu wangu, gari limepata pancha! Sijui mikosi yote hiyo inatoka wapi wakati ninapowania kupata kibali cha kuendesha gari. Nimeyaweka wapi mabamba ya tahadhari barabarani?

**22. SFX:** **opening boot of mini bus, sound of rummaging around**

**23. SAMUEL:** Ajabu! Nitaweka matawi ya miti barabarani kuwatahadharisha madereva wengine.

**24. SFX:** **Breaking branches, cars passing by**

**25. PEDESTRIAN:** Hujambo… Kwani huna mabamba ya tahadhari? Unajua askari polisi watakutoza faini wakikupata? Haya matawi hayafai kabisa kuwaonya madereva wengine barabarani.

**26. SAMUEL:** Sina la kufanya sasa hivi. Nitatumia hayo matawi hadi nitakapomaliza kubadilisha gurudumu hili …

**27. SFX:** **Horn honking… Car stopping**

**28. JOHN:** Hali vipi Samuel?…Una nini? Umepata pancha?

**29. SAMUEL:** Salama John. Kawaida, breki hazifanyi kazi, kisha juu yake ni pancha… Una mabamba ya kutoa tahadhari barabarani? Nachelea nisipatikane na askari polisi barabarani bila kitu cha kuonyea magari mengine.

**30. JOHN:** Naam. Lakini ufanye bidii unirejeshee haraka iwezekanavyo. Sipendi kuendesha gari bila mabamda hayo… hali kwenye barabara hizi haijulikani. Mara mtu huenda upate ajali na ukahitaji hayo mabamba. Ni hatari sana kutumia matawi ya miti pekee barabarani.

**31. SAMUEL:** **(taking triangles)** Asante sana John. Nitakurejeshea haraka iwezekanavyo.

**32. JOHN:** Mara moja hiyo…. Hawa askari polisi washafika.

**33. POLICEMAN:** Kuna tatizo hapa? Ni ajali?

**34. SAMUEL:** Aaah, hapana afande. Ni pancha. Kama unavyoona nimeweka mabamba ya tahadhari ili kuwaonya madereva wapunguze kasi za magari yao.

**35. POLICEMAN:** Tafadhali nionyesha nyaraka zako!

**36. SAMUEL:** Bila shaka, afande.

**37. SFX:** **Opening car door, slamming shut**

**38. POLICEMAN:** Mmm, sawa. Nadhani unajua kwamba muda wa bima yako unakaribia kumalizika. Ishughulikie mara moja. Na hiki ndicho kibali chako?

**39. SAMUEL:** Mmmm.

**40. POLICEMAN:** Nadhani utahitajika kugharamika zaidi kumaliza tatizo hili.

**41. SAMUEL:** Ninafahamu. Hiyo noti inatosha kumaliza tatizo hilo?

**42. POLICEMAN:** Naam, ni sawa badala yetu sisi kukupa malazi kwenye kituo chetu kizuri cha polisi. **(laughing)**. Fanya bidii ubadilishe gurudumu lako uondoke. Magari yanaendelea kusongamana.

**43. SAMUEL:** Ndio, afande. Nafanya hivyo hivi sasa.

**44. SFX:** **police car driving off**

**Scene Three: Garage/Car yard**

**45. SFX:** **Banging, hydraulics, cars being moved around**

**46. MECHANIC:** Lini mara ya mwisho ulipolipeleka gari lako kuchunguzwa na kukarabatiwa?

**47. SAMUEL:** Eeeee… Sina hakika… Pengine miaka miwili iliyopita!

**48. MECHANIC:** Nadhani ni hivyo. Gari lako lina matatizo chungu nzima. Breki hazifanyi kazi…zimekwisha kabisa. Na hiyo pancha nayo inabidi kuzibwa. Taa ya mbele ya kulia haiwaki. Unajua kwamba ungesababisha ajali nyingi kwa sababu ya kuwa na taa moja pekee? Madereva wanaokuja kwa upande wa mbele watafikiria kwamba gari lako ni pikipiki.

**49. SAMUEL:** Eeeh, lakini siku moja bila kufanya kazi ina maana kukosa fedha.

**50. MECHANIC:** Ajali zinakukosesha fedha nyingi zaidi! **(angrily)** Ninajua ninachokisema. Watu hupuuza hitilafu ndogo ndogo za magari yao… baadaye wanashangaa magurudumu yanapong’oka, injini zinakwama kisha wanaishia mikononi mwa polisi kwa kusababisha ajali … Unafahamu hayo?

**51. SAMUEL:** Mmmm.

**52. MECHANIC:** Zingatia ushauri wangu. Hakikisha kwamba gari lako linachunguzwa na kukarabitwa mara kwa mara. Hapo utatulizana akili. Ushauri wangu huu nakupa bure!

**END OF SCENE THREE**

**SHORT MUSIC**

**53. BEATRICE:** Naam, kama mlivyosikia kwenye kipindi cha tano cha mchezo wetu wa redio, Samuel anaendelea kukumbwa na masaibu kadha wa kadha barabarani. Pamoja nami hapa studioni huyu hapa George, mtaalamu wetu wa usalama barabarani. George karibu!

**54. GEORGE:** Asante.

**55. BEATRICE:** George, ajali nyingine inamkumba Samuel na mara hii kwa sababu ya kutolitunza vizuri basi lake. Mambo yanaelekea kumwendea mrama!

**56. GEORGE:** Hapana waweza kusema kwamba ana mkosi. Lakini tukizingatia hali ya barabara barani Afrika – mashimo, lami mbovu, misongamano ya magari – magari yanakabiliwa na matatizo chungu nzima kwa hivyo yanatawa kukaguliwa na kukarabatiwa mara kwa mara. Fikiria ingekuwaje kama basi lake lingekuwa limejaa abiria wakati breki zilipokwama?. Ningependa kuwashauri wenye magari kuyakagua na kuyakarabati magari yao kila baada ya miezi sita.

**57. BEATRICE:** Na vifaa vya kimsingi vya usalama ambavyo inambidi mtu kuwa navyo kwenye gari… Unaweza kuligusia hilo?

**58. GEORGE:** Kwanza mabamba mawili ya kutoa tahadhari gari linapoharibikia barabarani. Unatakiwa kuyaweka mabamba hayo mbali kidogo na gari lakini ili madereva wanaokuja wapate kuona. Si kwa sababu ya usalama wao tu bali pia wako. Iwapo dereva anayekuja hawezi kupunguza kasi, huenda akagonga gari lako. Ni hatari.

**59. BEATRICE:** Lipi jengine ambalo msikilizaji anapaswa kulijua?

**60. GEORGE:** Ni lazima kuhakikisha gurudumu la ziada linapaswa kuwa katika hali nzuri na jeki kwa ajili ya kubadilisha magurudumu. Pia oili ya ziada pamoja na maji.

**61. BEATRICE**: Lakini George, mbona madereva wengi hawayatunzi magari yao vizuri? Twajua vyema kwamba kitu usipokitunza vizuri kitaishia kuharibika.

**62. GEORGE:** Nadhani hali hiyo inatokana na watu kutofikiria maisha ya usoni. Watu wengi wanajali maisha ya leo tu. Ninahitaji fedha leo kwa hivyo nikiondoa gari langu barabarani sitapata fedha. Ukilifanyisha kazi gari lako bila kulitunza, litaishia kuharibika na hapo utagharamika zaidi. Na hapo ninazungumzia upande wa kiufundi – usalama wa abiria ndio muhimu zaidi. Kama unabeba abiria, ni lazima gari lako liwe zuri na salama. Hilo ni jukumu lako.

**63. BEATRICE:** Asante , George.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**OUTRO**

**64. BEATRICE:** Katika kipindi kijacho tutasikia jinsi mama yake Pamela, ambaye anazidi kuzeeka, anapokabiliana na safari ndefu ya basi kutoka vijijini kwenda mjini katika mchezo mwingine wa redio ulioandikwa na Victoria Averill. Kama ungependa kusikiliza kipindi hiki kwa mara nyingine, basi tazama wavuti wetu www.dw.de/lbe. Asante sana kwa kujiunga nasi na jitahidi kuweka usalama barabani!